Jina …… Namba Yako ……

Shule …….

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
(FASIHI)
Julai / Agosti 2008
MUDA: Saa 2 ½

MTIHANI WA MWIGO WILAYA ZA HOMABAY SUBA - 2008
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI – (K.C.S.E)

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
(FASIHI)
Julai / Agosti 2008
MUDA: Saa 2 ½

MAAGIZO:
- Jibu maswali manne pekee
- Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi Simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa
Watahiniwa lazima wahakikishe kurasa zote zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU YA A

HADITHI FUPI

MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINE

1. Mkimbizi (John Habwe)

a) Maisha ya mkimbizi yametawaliwa na mkururo wa mikasa. Thibitisha al 14

b) Eleza sifa zozote za msimulizi wa hadithi hii al 6

2

SEHEMU YA C TAMTHILIA

KIFO KISIMANI; KITHAKA WA MBERIA

4. "Yaliyopita hurejea. Amekutaja tena jana. Aliniambia nikuambie umuone. Ni bahati nzuri tumekutana leo"

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.

b) Eleza sifa za anayeambiwa maneno haya . al 8

c) Eleza jinsi wanawake walivyochangia katika ukombozi wa Butangi. al 8

AU

5. Butangi ni kielezo cha mataifa mengi yanayoendelea . Jadili al 20

SEHEMU YA D USHAIRI

6. **Soma shairi hili kisha uyajibu maswali yanayofuatia**

1. Mvua iliyonyesha, ya maradi na ngurumo
   Kutwa na kucha kukesha, kunyesha pasi kipimo
   Haikuwanufaisha , wenye kazi za Kilimo
   Wenye kazi za vilimo , walifikiwa na hasara

2. Mimeya walioipanda , ilitekukatekuka
   Kazi ngumu waliotenda , yote ikaharibika
   Hawakuvuna matunda , waliyo wakiyataka
   Waliyo wakiyataka , yakawa mbali nao

3. Wenye kuicha mvua , isiwatose mwilini
   Baadhi yao wakawa , wakimbiliya pevuni
   Wengine hawakutuwa , hadi mwao majumbani
   Hadi mwao majumbani , na kukomeya milango

4. Wenzangu dhihaka kando, nisemayo ni yakini
   Ulibwaga kubwa shindo , mvua hiyo jamani
   Na mijaji kwa Mikondo, yakawa barabarani
   Yakawa barabarani, mvua kwisha kunyesha.

5. Kunyesha iliposiya, kukatapakaa tope

Zilijaa kila ndiya, isibakiye nyeupe
Ukawa mwingi udhiya , pa kupita zisitupe
Pa kupita zisitupe, kwa ndiya kukosekana

6. Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki
Bali mimi huamuwa, kwenda japo kwa dhiki
Kumbe vile nitakuwa , ni mfano wa samaki
Ni mfano wa samaki , kuiendeya ndowana

7. Zikanibwaga telezi , sikujuwa kuzendeya
Ningekwenda kwa henezi , yasingenifika haya
Lakini tena siwezi, mwendo huo kutumiya
Sitawata kutembeya , ila tabadili mwendo.

1

a) Kwa kuzingatia vina, shairi hili ni la bahari gani ? Al 2
b) Eleza dhiki zilizosababishwa na mvua
c) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili Al 4
d) Huku mkitolea mifano onyesha uhuru wa msanii unaojitokeza al 3
e) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari al 4
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumika katika shairi
- Kuicha
- Iliposiya
- Henezi al 3

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

1. a) Fasihi simulizi ina makundi manne makuu, yataje. al 4

b) Kwa kila kikundi ulichotaja katika swali la 1 (a) , toa mifano miwili ya vipera vya kila kikundi na utoe maelezo mafupi ya vipera hivyo al 8

c) Nyimbo huwa na jukumu gani katika usimulizi al 2

d) Fasihi simulizi ina sifa ya kuhifadhiwa akilini . Eleza udhaifu wa uhifadhi wa akilini. Al 6